

75.522 kwa Mkoaa wa Morogoro tangu imeingia madarakani kwa ajili ya ku-

hayo juzi mjini Morogoro wakati akitoa taarifa ya wiki ya utekelezaji wa miradi ya

HABARI LEO

mbalimbali za maendeleo pamoja na huduma mbalimbali za wananchi katika mkoa

UK 21

ngawo wa fedha za tozo ya miamala ya simu kwa kupatiwa Sh bilioni 1.637.



N
To

Rombo walia mifugo ya nchi jirani kuvamia mashamba yao

**Na Upendo Mosha,
Rombo**

WANANCHI wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro wameiomba serikali kuingilia kati tatizo la mifugo kutoka nchi jirani ya Kenya kuvamia mashamba na kuharibu mazao yao.

Wananchi hao walitoa kilicho chao hicho wakati wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye muktarano wa hadhara wa Mbunge wa Jimbo hilo, Profesa Adolf Mkenda wa kusikiliza kero katika Kijiji cha Keni, Kata ya Kiruakeni wilayani humo.

Mmoja wa wananchi hao, Justina Mroso, alisema wanaiomba serikali kuingilia kati suala hilo ili kuwanus-

uru na janga la kukosa chakula.

"Mwaka huu tumelima alizeti katika ukanda wa chinii na zimeota vizuri, tatizo ni wafugaji kuingiza mifugo na kula mazao yote hatukuambulia hata majani, hii inaumiza sana tunaomba serikali yetu kuliangalia hili," alisema.


Mwananchi mwingine, Bertha Faus-tine, alisema wafugaji kutoka nchi jirani ya Kenya huingiza mifugo kwenye mashamba kwa lengo la kupata malisho.

"Ni kama tunalima kwa ajili ya wafugaji

badala ya kulima kwa ajili ya kuingiza kipato pamoja na chakula," alisema.

Aidha, wananchi hao waliomba serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia mbegu bora zitakazowasaidia kulima kilimo chenye tija ili kuwekeza kwenye viwanda vya kukamua mafuta wilayani humo.

Kaimu Mkurugenzi wa



Halmashauri ya Rombo, Emmanuel Sindiyo, alisema wameshaanza kulishughulikia suala la mifugo ya nchi jirani kuingia nchini na kuharibu mazao ya wakulima.

"Ni kweli jambo hilo lipo, halmashauri imeanza kulishughulikia kwa kuitisha vikao na nchi jirani ili kupata utatuizi, tunaomba wananchi wawe wavumilivu wakati serikali inaendelea kulifanyia kazi," alisema.

Mbunge wa Jimbo hilo na Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, alisema ni lazima jithada za makusudi zichukuliwe kuhakikisha suala la mifugo ya kutoka nchi jirani linapatiwa ufumbuzi.

**Kil
40C
Na Mwa**

MCEF), urri ya Wil mkoani I milioni 4 di mbali la kupun rasilimal

Wilay pokea ru mwaka 2 wa fedha Sh milio mfuko k maendel tekelezew

Kwa Mkurug halmash Mwingi ambayo inayopae Udzung